

## **Tathmini ya Mikakati ya Tafsiri ya Vinay na Derbelnet (2004) katika Tafsiri ya A Good Day (2019)**

*Sarah Ndanu M. Ngesu<sup>1</sup>, Pendo Salu Malangwa<sup>2</sup> na Mosol Kandagor<sup>3</sup>*

<sup>1</sup>*Chuo Kikuu cha South Eastern Kenya*

<sup>2</sup>*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

<sup>3</sup>*Chuo Kikuu cha Moi*

### **Ikisiri**

Uteuzi wa mikakati ya tafsiri katika mchakato wa tafsiri, ni suala muhimu katika Nadharia ya Tafsiri. Lengo la makala haya ni kutathmini mikakati ya tafsiri iliyotumiwa katika kutafsiri ya riwaya ya Kiswahili *Siku Njema* iliyotafsiriwa kwenda Kiingereza kama *A Good Day*. Uteuzi wa mikakati ya tafsiri unaweza kuwa na athari zake katika uhawilishaji wa ujumbe. Hata hivyo, suala hili halijapewa nafasi inayostahiki katika tafiti tangulizi kuhusu kazi za tafsiri. Tathmini za tafsiri hujikita kuchanganua changamoto za tafsiri bila kuonesha kwamba uteuzi wa mikakati ya tafsiri una mchangano mkubwa katika kuibua changamoto hizo. Modeli ya Vinay na Derbelnet (2004) ilitumiwa kubaini mikakati ya tafsiri iliyotumiwa na wafasiri Dorothy Kweyu na Fortunatus Kawegere. Wataalamu wanakubaliana kwamba Modeli ya Vinay na Derbelnet ndio msingi wa uainishaji wa mikakati ya tafsiri na wataalamu wengine wanaoainisha mikakati ya tafsiri hutumia modeli hii kama msingi wa uainishaji wao.

**Maneno Muhimu:** Mikakati ya Tafsiri, *Siku Njema*, *A Good Day*

### **Utangulizi**

Ijapokuwa tafsiri huonekana kama mchakato wa kuhamisha ujumbe kutoka lugha chanzi hadi lugha lengwa, kulingana na Nida na Taber (1969), tafsiri ni mchakato unaohusisha mambo mengi. Mihimili mikuu ya tafsiri ni kufanya uchanganuzi, kuhawilisha na kuandika upya ujumbe kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa. Katika hatua ya uchanganuzi, mfasiri huchunguza kwa makini muundo wa ujumbe wa lugha chanzi, maana ya maneno, vishazi na sentensi ili kumwezesha kuelewa ujumbe mzima. Hatua ya pili ni kuhawilisha ujumbe kama alivyouelewa kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa. Hatua ya tatu na ya mwisho ni kuhakikisha uhawilishaji wa ujumbe umekitwa katika muktadha wa hadhira lengwa. Kulingana na Larson (1984), vipengele muhimu katika mchakato